# Wafanyakazi wa India Wanalinda Chuma Chao Kwa Uhai Wao: Jarida la Thelasini na Nne (2022)




Marafiki Wapendwa,

Salamu toka dawati la Tricontinental: Institute for Social Research.

Kipindi kirefu cha kabla-ya-historia kinatajwa kuwa ni kipindi chote cha kabla ya wakati wa kawaida, ambacho kikawaida hugawanywa katika vipindi vitatu: zama za mawe, zama za shaba na zama za chuma. Baadaye, katika kipindi cha historia iliyoandikwa, kwa jumla hatukutegemea aina fulani pekee ya metali na madini kufafanua zama. Madini na metali za aina nyingi,


yakiwezeshwa na mbinu mpya za uzalishaji na mnyororo wa nguvu-kazi, yamechangia vilivyo kwa katika kukuza uwezo wetu wa kuzalisha ziada kubwa. Kuna zama za viwanda lakini, kwa mfano, sio zama za chuma-chakatwa(steel) , metali iliyo kiini kwa zama zetu.

Mwaka 1914, mshairi mmoja wa Urusi aitwaye Alexei Gastev aliandika, ‘Tunakua kutokana na chuma’. Ninatizama vinu vya kufulia na kuhunzi, nyundo na mitambo na kisha:

> Ninapoikodolea macho, ninasimama wima vema.
> Mishipa yangu ya damu inatiririsha kitu kipya, damu ya chuma,
> Na kisha ninaanza kukua.
> Ninayakuza mabega ya chuma vilivyo na mikono imara.
> Nimeunganishwa na chuma.
> Kwa mabega yangu, ninasukuma nguzo mpaka juu darini.
>
> Miguu yangu imekita ardhini, lakini kichwa changu kipo juu zaidi ya jengo.
> Na wakati bado ninakabwa na jitihada zisizokuwa za kibinadamu,
> Tayari ninalia:
> neno, makamaradi,neno!
> Mwangwi wa chuma umesikiliza maneno yangu, jengo lote latetemeka pasi simile.
> Ninazidi kuinuka juu; nipo ngazi sawa na mabomba.
> Na hapa hakuna habari, hakuna hotuba.
> Kuna kilio pekee:
> Tutashinda!


SAVE
VIZAG

Virusi vya kuacha uzalishaji wa viwandani vilivyojikita Amerika ya Kaskazini na Ulaya miaka ya 1970 vilizalisha fikra za kiuanazuoni kuhusu *'jamii ya baada ya viwanda'.* Fikra na maandiko haya yalipelekea dhahania kwamba uchumi wa kidijitali utakuwa injini ya msingi ya kulimbikiza mtaji; kulikuwa na kujali kudogo juu ya hoja kuwa hata uchumi wa kidijitali unahitaji miundombinu, ikiwamo satelaiti na nyaya za chini ya bahari pamoja na vituo vya uzalishaji umeme na vifaa vingine kwaajili ya kulinganisha na kuunganisha njia za dijitali. Uchumi huu wa kidijitali unasimama kutokana na metali na madini mbalimbali – kuanzia shaba mpaka lithium. Chuma, kichakatwacho katika viwanda vikubwa, kimeendelea kuwa nguzo katika jamii yetu. Chuma hiki – kilicho imara mara maelfu zaidi ya madini ghafi ya chuma(iron ore) – kinapatika mahala pengi katika Dunia yetu kama ilivyo plastiki.




Visual Capitalist, *Miaka 50 ya uzalishaji Global Steel katika picha*, 2021.

Kwa takribani miaka 50 iliyopita uzalishaji wa chuma umeongezeka mara tatu. Wazalishaji wakubwa wa chuma kwa sasa ni China, Ulaya, India, Japan, Urusi na Marekani. Katika kipindi cha janga la kiulimwengu la UVIKO -19, uzalishaji wa chuma ulipungua kwa kiasi cha 1%, kwa kiasi kikubwa ilitokana na mahitaji ya ndani katika nchi za China na India zilizosababisha vinu vyao vya kufulia chuma kuendelea kufanya kazi. Wakati uzalishaji wa chuma nchini China ulipungua kwa wastani kwa sababu ya hofu ya uzalishaji-ziada, viwanda vya chuma vya India vimeongeza uzalishaji wa chuma katika kipindi cha janga la kiulimwengu la UVIKO -19.

Viwanda vingi kati ya viwanda vya chuma nchini India vipo katika sekta ya umma na vinaendeshwa na mashirika ya serikali. Miongoni mwa viwanda hivyo ni Rashtriya Ispat Nigam Limited (RINL), eneo la viwanda vya chuma huko Kusini -Mashariki katika jimbo la Andhra Pradesh.

Kiwanda kwa mapenzi huitwa 'Visakha Steel', kilizaliwa kutokana na mapambano ya umma yaliyoongozwa na watu wa Andhra Pradesh yaliyoanza mwaka 1966 na kudumu mpaka vinu vya kufulia chuma vilipowashwa mwaka 1982. Eneo la kiwanda liasisiwa nyakati ambazo dola la India lilikuwa chini ya mgandamizo mkubwa kutoka katika tabaka tawala la India pamoja shirika la fedha la kimataifa (IMF) na kuanza kuufanya uchumi kuwa wa kiliberali (kulegeza masharti ya kiuchumi) hususani kwa kupitia ubinafsishaji wa mali za taifa. Hivyo kiwanda kilizaliwa katikati ya ulimwengu wa kiliberali, wakati serikali ikiwa imenuia kuongeza kwa makusudi uwezekano wa kukiuza kiwanda kile kwa mtaji binafsi katika wimbi la ubinafsishaji ambalo baadaye lilikuja kuitwa uharamia (piratisation).


CITU
VIZAG STEEL
SAVE STEEL PLANT

Habari ya kuhamasisha ya Visakha Steel ni mada katika dozia yetu no 55 (ya Agosti 22), *Kiwanda Cha Chuma Cha Watu na Mapambano Dhidi ya Ubinafsishaji huko Visakhapatanam*. Dozia inafafanua mapambano ya watu wa Andra Pradesh kuishurutisha serikali kujenga kiwanda, 'hekalu la India mpya ', kama ambavyo waziri mkuu wa kwanza wa India Jawaharlal Nehru alivyowaita. *Visakha Ukku, Andhrula Hakku* vijana na wanafunzi walipiga kelele: 'Visakha Steel ni haki ya watu wa Andhra'. Mwaka 1966, mapambano hayo yalikumbana na vurugu kubwa toka kwa dola ambayo ilipelekea vifo vya watu thelasini na wawili na kukamatwa na kuteswa kwa wengine wengi. Baada ya kushindwa kuliangamiza vuguvugu lile ambalo lilipewa sura na uelekeo na wakomunisti , na uelewa juu ya unyeti na ulazima wa uzalishaji wa chuma kwa India iliyokuwa ikihaha kutafuta kuyavuka matatizo ya njaa na elimu, serikali iliridhia kujenga kiwanda cha ilitumia Rupee za India bilioni 17 katika kipindi cha miaka ya 1970 kuanza ujenzi wa kiwanda.

Tangu Visakha Steel iibuke nyakati ambazo 'dini' ya ubinafsishaji ilikuwa imeshika kasi, serikali ya India kwa nyakati tofauti ilijaribu kuhujumu uwezo wake wa kusalia katika sekta ya umma kwa kuzuia kiwanda cha chuma kupata migodi inayoshikiliwa, kujenga bandari binafsi karibu na Gangavaram,kujenga uwezo na ufaninisi katika kitengo cha uyeyushaji (kuchakata madini ghafi ya chuma kuwa chuma),na kupata kwa wakati ruzuku za serikali. Badala yake serikali ilijaribu kuacha kampuni binafsi kuunda vitengo vya uyeyushaji chuma ambavyo vilikuwa vikitumia chuma kilichoongezewa thamani kutoka Visakha Steel kwaajili ya kuunda chuma kilichochakatwa ambacho huuzwa kwa faida maradufu, hatua ambayo wafanyakazi waliishinda. Hata mara moja serikali haikuonesha jitihada za kuongeza na kuboresha uzalishaji wa chuma ama kuboresha mazingira ya wafanyakazi wa kiwanda cha chuma na familia zao.



Kwa upande mwingine, wafanyakazi, walikuwa na mawazo yao. Wakiongozwa na Kituo Cha Vyama vya Wafanyakazi India (Center for Indian Trade Unions,CITU) na vyama vingine vya

wafanyakazi, wafanyakazi walipambana kurekebisha mikopo ya serikali kuwa gawiwo la serikali , na kuutoa mgodi wa madini ya chuma ulioshikiliwa na kiwanda, na kujenga uwezo katika kitengo cha uyeyushaji chuma. Kama ambavyo dozia yetu inavyoanisha , wafanyakazi wa sekta ya chuma wamekuwa 'wakijitoa kwa nguvu kwaajili ya ukuaji wa kampuni ili kiwe kama kiwanda chenye mbinu imara na chenye stahimili ya hesabu kifedha, iwe katika kupambana kutanua kiwanda, kupata migodi iliyoshikiliwa ama kushughulika matatizo na masuala ya kiufundi. Yanapotokea matatizo ya kiufundi katika kiwanda, yawe ya umeme, kitengo cha uyeyushaji ama mengineyo, wafanyakazi na vyama vyao wametafiti Kwa kina bila kuchoka na kufanya uchambuzi na kuja na majawabu mujarabu'. Tulichonacho hapa ni serikali yenye kiu ya kukifanyia umumiani Visakha Steel na wafanyakazi waliojidhatiti katika uzalishaji katika 'Kiwanda Cha Chuma Cha Watu'.

Badala ya kuifanya bandari ya Gangavaram kuwa sekta ya umma kama ilivyokuwa ikitarajiwa, serikali imelipa kampuni binafsi la Adani Group – ambalo mmiliki wake ana mahusiano ya karibu na Waziri Mkuu Nerandra Modi – kampuni ambo linaitoza Visakha Steel ada na tozo kubwa. Ni muhimu kuweka kumbukumbu kuwa bandari hii ilijengwa katika ardhi iliyokuwa ikimilikiwa na kiwanda cha chuma. Zaidi , licha ya kuwa Visakha Steel wanalipa kodi za majengo katika jiji, bandari binafsi ya Adan Group wana msamaha wa kodi. Wakati huohuo , serikali ya Waziri Modi ilikwishajaribu kuikabidhi ardhi ya Visakha Steel.kwa kampuni kubwa la chuma la nchini Korea Kusini liitwalo POSCO ili iweke mitambo yake ya kuunda bidhaa za chuma zilizoboreshwa zaidi(auto grade steel products) kwa kutumia chuma kinachotoka kiwanda cha Visakha. Katika mtindo uliozoeleka wa ubinafsishaji kwa usio kikomo , dozia inafafanua, ' Visakha Steel ilitakiwa kushughulikia shughuli ambazo ni tata, za hatari na za ' kichefuchefu' -manunuzi ya madini ghafi ya chuma, kuendesha mitambo ya ukaangaji wa madini ghafi ya chuma, planti za oksijeni, na vinu mbalimbali vya ufuaji- wakati POSCO ilifanya kazi katika maeneo rahisi na yenye faida kubwa katika myororo wa uzalishaji'.



Hakifanyiki chochote, walizungumza wafanyakazi. Wakizingatia mapambano yaliyopelekea ujenzi wa kiwanda kwanza, wafanyakazi walianza vuguvugu kuikomboa Visakha Steel. Wimbo la vuguvugu hili – ambalo lilipata uungwaji mkono wa muhimu kutoka kwenye mapambano ya wakulima, chama cha wafanyakazi wa malezi ya watoto wa vijijini, -na watu wa Andhra Pradesh – wakiuzuia mkono wa serikali. Wakati serikali ikiwa imeharibikiwa wakati wa janga la kiulimwengu la COVID-19, walikuwa ni wafanyakazi wa sekta ya chuma walioweza kuendelea kuendesha mitambo yao ya oksijeni na kuzalisha oksijeni inayokubalika kitabibu kwaajili ya hospitali mbalimbali.

Hayaandikwi mengi yanayotuhusu mapambano kama haya, yanayoongozwa na wafanyakazi wa sekta ya chuma ambao mara nyingi husahaulika ama,ikiwa watakumbukwa, watazodolewa. Wanasimama kando ya vinu vya kufulia chuma, wakiunda na kukunja chuma, kukifanisi, wakisaidia ujengwaji wa mifereji bora ya umwaguliaji kwa wakulima, wakisaidia ujengwaji wa nguzo za shule na hospitali, na wakisaidi ujengwaji wa miundombinu Ili basi watu wa jamii Yao waweze kuvuka vigingingi vinavyoukabili utu. Dozia yetu inajengwa kupitia makutano na mijadala yetu na wafanyakazi wa sekta ya chuma na chama chao,ambao walitufahamisha namna ambavyo wanaielewa historia yao na namna wanavyoyaelewa mapambano yao. Na walitupatia picha zao (sambamba na picha zilizopigwa na Kuchem Rajesh wa gazeti lililopo Andhra Pradesh liitwalo *Prajasakti*), ambapo humo kitengo chetu cha sanaa kiliunda jopo lililoipamba kwa michoro dozia (michache imewekwa katika jarida hili).

Wakati wa maandano yao, wafanyakazi huimba nyimbo za hamasa na kutamba mashairi yanayowahimiza wao kujiandaa na mapambano 'kabla dunia haijapotelea chini ya miguu yetu, kabla chuma hakijateleza na kuondoka mikononi kwetu', 'jiji la Visakha litageuka kinu cha kufulia chuma ,na Andhra Kaskazini itageuka uwanja wa mapambano endapo mtajaribu kubinafsisha kiwanda hiki, wafanyakazi waliimba.....Tutakilinda chuma chetu kwa uhai wetu.'

Kwa huba,

Vijay

*Jarida hili limetafsiriwa katika lugha ya kiswahili na,* **Muhemsi Mwakihwelo.**